**1.0 Jina la Mradi:** Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula (LDFS)

- Mradi huu ni miongoni mwa miradi kumi na mbili ya majaribio inayotekelezwa katika nchi kumi na mbili zilizo kusini kwa Jangwa la Sahara. Nchi hizo ni Kenya, Ethiopia, Uganda, Burundi, Tanzania, Eswatini, Malawi, Nigeria, Ghana, Bukina Fasso, Niger na Senegal.
- Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu zinatolewa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility- GEF*) kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 7.156 na kusimamiwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*International Fund for Agricultural Development - IFAD*).
- Fedha za ndani (*Co-financing*) ni Dola za Marekani milioni 42 kati ya hizo Dola za Marekani 13,000.00 ni taslimu zilibaki.
- Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai 2017 hadi Septemba 2022 na ulizinduliwa rasmi tareh 23 Machi, 2018.

**2.0 Malengo ya Mradi**

- Kuboresha mifumo ikolojia ya kilimo ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji wa chakula na kuchangia kuboresha mazingira katika Halmashauri za wilaya husika.
- Kuboresha usimamizi endelevu wa mifumo ikolojia inayochangia kutoa huduma muhimu za uzalishaji kwenye maeneo ya ardhi, maji, misitu, bioanuai kwa madhumuni ya kuboresha uzalishaji.

**3.0 Maeneo ya utekelezaji wa Mradi**

- Mradi unatekelezwa katika maeneo yenye changamoto kubwa za uharibifu wa mazingira hasa mmonyoko wa udongo, kupungua kwa rutuba ya udongo, uharibifu wa vyanzo vya maji na misitu zilizopo katikati ya nchi na pwani.
- Maeneo ya utekelezaji wa mradi ni katika Kata ya Haubi (vijiji vya Haubi na Mafai) katika Halmashauri ya wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma; Kata ya Sigili (vijiji vya Sigili, Bulenda, Bulambuka, Lyamalagwa na Iboja) katika Halmashauri ya wilaya ya Nzega, mkoani Tabora; Kata ya Mpambala (vijiji vya Mpambala, Nyahaa, Lugongo, Mkiko na Munguli) katika Halmashauri ya wilaya ya Mkalama, mkoani Singida; Kata ya

Sukuma, (vijiji vya Iseni, Lumeji na Nyang'hanga) katika Halmashauri ya wilaya ya Magu mkoani Mwanza na Kata ya Michweni na Kiuyu Maziwa Ngombe, (shehia za Michweni mjini, Michweni chamboni, Kwale/Majenzi, Shumba mjini, Maziwa ng'ombe, Kiuyu Mbunyuni, Mjini Wingwi na Shanake) katika wilaya ya Michweni, mkoa wa Kaskazini Pemba.

- Vigezo vya kuchagua maeneo haya vilikuwa ni ukame, mvua za wastani, upatikanaji mdogo wa chakula na utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano.

## 4.0 Kazi zilizopangwa kutekelezwa chini ya mradi huu.

- **Eneo la Kwanza *(Component 1)*** – Kujenga Uwezo wa kitaasisi katika Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Hifadhi ya Bioanuai katika eneo husika. Lengo ni kusaidia utekelezaji wa mradi hasa kwa kujenga uwezo kwa watendaji wa mradi katika ngazi ya vijiji/shehia, kata, wilaya na taifa ili kuweza kusimamia na kutekeleza shughuli za mradi.
- **Eneo dogo la kwanza 1.1:**
  Uanzishwaji wa Kamati za Uwakilishi za vijiji/shehia na kufanya utambuzi wa watumiaji wote wa maliasili kwa kushirikisha vijiji/shehia vinavyopakana.
- **Eneo dogo la kwanza 1.2**
  Kuandaa mpango mahususi wa matumizi ya ardhi ya vijiji/shehia na kuanzisha taratibu za kisheria za usimamizi wake kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Kamisheni ya Ardhi ya Zanzibar na kutoa Hati Miliki za Kimila.
- **Eneo dogo la kwanza 1.3**
  Kufanya mapitio ya mipango ya vijiji/shehia iliyopo, taasisi zilizopo na kutambua mahitaji halisi ya mafunzo yanayohitajika katika Kamati za Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Kamati za Usimamizi Maliasili za vijiji/shehia.
- **Eneo dogo la kwanza 1.4**
  Kufanya mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Kamati Shirikishi za Usimamizi wa Mazingira na Maliasili, wilaya na watendaji wa vijiji/shehia na jamii kwa utaratibu wa kujifunza na kutekeleza.

- **Eneo dogo la kwanza 1.5**
  Kuwezesha makubaliano ya kwenye matumizi ya ardhi, upatikanaji wa hifadhi ya rasilimali na matumizi ya miongozo kwa makundi mbalimbali kwa kuboresha/kupitia mifumo ya uongozi na sheria ndogo zilizopo.
- **Eneo dogo la kwanza 1.6**
  Kuweka vipaumbele kwa makundi yanayosaidia urejeshwaji wa uoto na ardhi iliyoharibika na hifadhi ya bionuai.
- **Eneo dogo la kwanza 1.7**
  Kutambua teknolojia na maeneo ya yanayofaa kwa uvunaji wa maji; maeneo ya vyanzo vya maji na usimamizi wa vyanzo vya maji katika vijiji/shehia. Lengo ni kuwezesha jamii kupata maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo na mifugo.

**Eneo la pili (*Component* 2)**

Kuendelea kuboresha kilimo hifadhi na rafiki kwa mazingira, hifadhi ya ardhi, hifadhi ya maji na usimamizi wa mifumo ya nyanda za malisho.

- **Eneo dogo la pili 2.1**
  Kuandaa mafunzo ya shamba darasa kwa wakulima kuhusu kilimo hifadhi na mbinu bora za kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kilimo hiki kitahusisha kilimo hifadhi, uboreshaji na urutubishaji wa udongo, mbinu za kilimo misitu, kilimo cha makinga maji, kilimo cha mzunguko, usimamizi shirikishi wa kudhibiti wadudu na magonjwa ya mazao. Mafunzo haya yatakwenda sambamba na kuwasaidia wakulima katika upatikanaji wa mbinu bora za kilimo na pembejeo kwa wakulima katika mashamba darasa yatayoanzishwa.
- **Eneo dogo la pili 2.2**
  Kuandaa mafunzo ya vikundi vya watumia maji na watunzaji vyanzo vya maji kwa wakulima, wafugaji na wananchini kuhusu uvunaji maji na ukarabati au uchimbaji wa mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo, mifugo na matumizi ya jamii. Kazi kuu zitahusisha ukarabati wa visima na mabwawa/ujenzi na uchimbaji wa mabwawa mapya ya kuhifadhi maji, visima, ununuzi wa matanki ya kuhifadhi maji na kutambua maeneo ya vyanzo vya maji na kuweka taratibu za usimamizi wake. Vilevile kutumia mabwawa kwa ufugaji wa samaki.

- **Eneo dogo la pili 2.3**
  Kuandaa mafunzo ya shamba darasa kwa wakulima na wananchi kuhusu utunzaji wa vitalu vya miti na usimamizi endelevu wa misitu. Kuendesha mafunzo kwa ajili ya kuhimiza matumizi ya nishati mbadala kwa ajili ya kupikia na majiko banifu ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa kupikia kwa kiwango kikubwa.
- **Eneo dogo la pili 2.4**
  Kuandaa mafunzo ya shamba darasa kwa wafugaji kuhusu njia bora za uendelezaji nyanda za malisho na ufugaji wa kisasa. Baadhi ya kazi zitakazofanyika zinahusiana na kuboresha nyanda za malisho zilizopo kwa kuondoa malisho yasiyohitajika, kupanda aina nzuri ya malisho (species) katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kulingana na Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi ya Vijiji/shehia. Kukuza na kuendeleza mbinu za asili ya kuhifadhi malisho za Ngitiri katika maeneo yasiyo tumia mbinu hizi za asili kwa kutenga maeneo. Kuboresha ufugaji wa samaki katika mabwawa na kandokando vya fukwe za bahari hasa katika maeneo ya Micheweni. Kujenga na kukarabati majosho ya mifugo katika maeneo ya wafugaji.
- **Eneo dogo la pili 2.5**
  Kuandaa mafunzo ya shamba darasa kwa kutumia njia mbadala za kuongeza kipato kwa wakulima, wafugaji na wawindaji. Baadhi ya kazi zitahusisha kutoa mafunzo ya kuongeza thamani ya mazao hasa uchakataji na ufungashaji, upatikanaji wa mizinga ya kufugia nyuki, kuboresha maeneo ya asili kwa ajili ya kuvutia watalii, kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuanzishwa biashara baada ya kufanya tathmini ya kina ya aina ya biashara za kufanyika.

**Eneo la Tatu (*Component 3*)**

- Ufuatiliaji na Tathmini. Dhumuni la eneo hili ni kujenga uwezo kwa watendaji wa halmashauri na Kamati Shirikishi za Vijiji/Shehia za Usimamizi wa Mazingira na Maliasili kuweza kutumia nyenzo za kufanyia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi.
- Vilevile utahusisha utafiti kwa ajili ya kupata taarifa za msingi na awali za eneo la mradi (*Baseline study*), utafiti wa upatikanaji wa taarifa za hali

halisi ya maeneo ya mradi kabla na kufanyika kwa shughuli za mradi (*Biophysical Assessments*), uandaaji wa ripoti za fedha na za utekelezaji wa mradi kwa vipindi mbalimbali na ukaguzi wa ndani na wa nje wa fedha na shughuli za mradi, ukaguzi wa kimataifa wa mradi (*IFAD/GEF mission*), kufanya ziara za kubadilishana uzoefu ndani na nje kwa kuhudhuria mikutano inayoandaliwa na Ofisi ya kikanda ya uratibu wa mradi (Regional Project Hub), ziara za ndani kwa watendaji na wanakamati, wanavijiji/wanashehia za kijifunza na kubadilisha uzoefu, kuandaa mbinu bora za mafanikio ya mradi (*Documenting Best Practices*) na kufanya ufuatiliaji wa mradi kwa kila robo mwaka.

**Eneo la Nne (*Component 4*)**

**Uratibu na Usimamizi wa Mradi.**

Eneo hili linahusu uratibu na usimamizi wa mradi. Usimamizi wa Mradi huu utakuwa chini ya Kamati ya Kitaifa ya Uongozi na Kamati ya Ufundi ya Ushauri ya Mradi. Shughuli za kila siku zitasimamiwa na timu ya uratibu wa mradi chini ya usimamizi wa Mkurugenzi wa Mazingira.